ZAIDI YA
ENEO LA GIZA

# MSAADA WA MAOMBI YA NENO LINALOTAMKWA

## SIKU YA KIMATAIFA YA MAOMBI KWA AJILI YA WAATHIRIKA WA USAFIRISHAJI WA BINADAMU

Waalike waumini wako wawashirikishe wengine maombi haya ya neno la kutamkwa kwa sauti kwa kuwatizama wanusurika, waathirika, washirika na wabia. Unaweza vile vile ukawaonyesha video ya maombi ya neno la kutamkwa iliyotayarishwa kwa ajili yako. Tunaomba maombi haya ya kutamkwa yasaidie kuleta huruma na mshikamano katika mioyo na ipelekee hatua kuchukuliwa.

### MAOMBI KUTOKA KWA MTIZAMO WA MNUSURIKA

Tunatakiwa kuzisikiliza sauti za ustahimilivu tunazoziombea. Kilio chao ni kipi? Hapa pana ombi la kutamkwa kutoka kwa mtizamo wa mmoja aliyeguswa na utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu. Unaweza vile vile ukaipata ile video hapa: #BeyondTheDark Human Trafficking Survivor Spoken Prayer – YouTube

*Mpendwa Mungu,*
*Kama mnusurika*
*Wananitizama*
*Nao waona mashine ya kutengeneza fedha,*
*Wananiona nikiwa dhaifu,*
*Nao wananiwinda.*
*Wanahalalisha nguvu zao*
*Kwa kutoheshimu uhuru wangu.*
*Haki zangu za binadamu hazina maana kwao,*
*Nao huamua juu ya hatima yangu.*

*Sio yangu tuu,*
*Bali hatima ya familia yangu.*
*Wakati wengine wanauona mwangaza*
*Sauti yangu imefungwa gizani.*
*Imefanywa mtumwa wa mawazo yangu*
*Naufikiria ulimwengu ambao*
*Watu wako wanapambana kwa ajili ya uhuru wangu*
*Mahali ambapo hawatenganishi*
*Uwepo wangu na ule wa mtoto wao.*
*Unatuita sisi ni wamoja katika mwili wa Kristo*
*Na badala yake wanatugeuzia migongo*
*Wakisema sisi hatuna mahusiano.*

*Zaidi ya kucheza ngoma,*
*Mataa, vicheko,*
*Giza lingali lipo*
*Likifunga vilio vyangu na kuvifanya mateka.*
*Wanapitia haraka haraka katika kitabu cha Yoshua*
*Wakishangazwa na mji ulioanguka*
*Na badala yake wanasahau kuta za Yeriko*
*Zimeuzunguka uhuru wangu.*
*Nahitaji mkusanyiko wa askari.*
*Uliojaa kelele*
*Tayari kupaza sauti yangu.*
*Na nichukue silaha zangu*
*Nikivumilia muda utakaohitajika*
*Kwasababu hayatakuwa ya bure*
*Mpaka nitakapo simama mimi.*

### MAOMBI KUTOKA KWA MTU ALIYE KATIKA MAZINGIRA HATARISHI

Hapa kuna video ya maombi ya kutamkwa kutoka kwa mtizamo wa mtu ambaye yupo ukingoni na aliye katika mazingira hatarishi ya utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu. Unaweza vile vile kupata video hiyo hapa: #BeyondTheDark Vulnerable Spoken Prayer – YouTube

*Mpendwa Mungu,*
*Mimi nimo katika mazingira hatarishi ya kunyonywa.*
*Napenda sura yangu,*
*Wanasema mimi napendeza.*
*Kwa kifupi nastaajabu,*
*Kisha nang'amua,*
*Uso wangu gharama yake ni nini?*
*Je, itanigharimu uhuru wangu?*

*Mama alisema, onyesha heshima,*
*Waambie watu habari mama, habari baba*
*Wasichana wazuri hufanya hivi na tabasamu*
*Wasichana wazuri huwa hawana vitabia*
*Wasichana wazuri hawatakiwi kudhaniwa,*
*Sikiliza zaidi*

*Waite mjomba au shangazi.*
*Je, nitajenga mahusiano ambayo siwezi kuyatikisa?*
*Je, kuonyesha heshima au kuwa rafiki*
*kutafungua mlango wa mauti kwangu?*
*Je, watu watalipa fedha ili kutizama mateso yangu?*
*Wakichagua madakika ya furaha kwa mshangao wangu.*

*Lakini huenda nitakua na kuongezeka.*
*Je, mabadiliko ya maumbile yangu yatasababisha nilengwe?*
*Nisiwe salama mahali, mahali,*
*Kazini, shuleni, kanisani.*
*Bila ya kutimiziwa hitaji,*
*Mimi sina gharama?*

*Maisha yangu yana gharama gani?*
*Nilidhani ulinipa maisha haya bure?*
*Au ni ndoto za watoto?*
*Mpaka hofu yangu isiwe ni juu ya mwili wangu,*
*Usalama haujaunganishwa na kuitikia.*
*Uhuru hauko sambamba na kifo changu.*

# ZAIDI YA ENEO LA GIZA

# MSAADA WA MAOMBI YA NENO LINALOTAMKWA

## SIKU YA KIMATAIFA YA MAOMBI KWA AJILI YA WAATHIRIKA WA USAFIRISHAJI WA BINADAMU

*Ndipo umbo langu litaonekana*
*Kuwa ni shukurani kwa kazi yako.*
*Ni lini maisha yangu ya sasa, ndoto zangu, maisha yangu yajayo yatahifadhiwa?*

### MAOMBI YA KUTAMKWA YA ALIYE MSTARI WA MBELE

Haya ndiyo maombi ya kutamkwa kutoka kwa mtizamo wa mtu aliye mstari wa mbele katika mapambano – wale wote walioko duniani kote, wanaotembea na kusafiri na wanusurika wa utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu wakihakikisha haki za jamii zinatendeka kwao. Unaweza kupata hiyo video hapa: #BeyondTheDark Practitioner Spoken Prayer – YouTube

*Mpendwa Mungu*
*Kama mtu aliye mstari wa mbele ninayefanya kazi*
*kupambana dhidi ya usafirishaji haramu wa binadamu*
*Maombi yangu ni haya*
*Naomba mapenzi yako yafanyike hapa duniani*
*Kama sauti za kimya kimya*
*Zinavyolia kutoka ng'ambo ya giza.*
*Wakihitaji watambulike kwasababu ya utu wao.*
*Na mwanga ambao haupofushi macho lakini unaweka huru*

*Naomba mapenzi yako yatendeke*
*Yakiwa yamejaa neema*
*Wanapo tabasamu*
*Kumbukumbu maridadi ya nguvu zao*
*Hewa wanayoivuta*
*Sherehe ya uhuru*
*Ninapoona tumaini kwenye nyuso zao*
*likiwasha moto wa ibada yangu*

*Naomba mapenzi yako yatendeke*
*Kuna siku najiuliza swali itakuwaje,*
*Maisha yangekuwaje*
*Bila ya kudhalilishana*
*Bila ya unyonyaji*
*Bila ya kuvamiana*
*Bila ya unyanyasaji*
*Bila ya watu wako kuonekana kuwa ni mali ya watu wengine*
*Bila ya kupumua kwao kumtegemea mtu mwingine*

*Naomba mapenzi yako yatimizwe hapa duniani*
*Wakati kila mmoja atasimama na wenzie pamoja*
*Kuthamini maisha badala ya fedha*
*Wakati kila mmoja atasimama na wenzie pamoja*
*Ili kupaza sauti zao kwa vilio vya walioumizwa*
*Wakati kila mmoja atasimama pamoja na wenzie*
*Ili kuona mapenzi yako yakitendeka hapa duniani*
*Kama ilivyo mbinguni.*

### MAOMBI YA KUTAMKWA YA WABIA

Maombi ya kutamkwa kutoka kwa mtizamo wa watu wanaopenda kusimama kwa mshikamano na wale wanaopitia utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu. Unaweza kuipata hiyo video hapa: #BeyondTheDark Ally Spoken Prayer – YouTube

*Mpendwa Mungu,*
*Mimi ni mbia ninayejitahidi kuhakikisha haki inapatikana*
*Nitapambana,*
*Haja ya kuwa na starehe*
*Haja ya kuwa salama*
*Ujinga uliopo kuhusu maswala*
*Unaochangia usafirishaji uwepo*

*Nitaacha*
*Kujihusisha katika starehe*
*zinazompa mkandamizaji nafasi na faida*
*Wakati dada zangu na kaka zangu*
*Wanapoteza sauti zao*
*Utu wao*
*Utambulisho wao*
*Tumaini lao*

*Nitahakikisha*
*Kabla sijaunga mkono kampuni yoyote*
*Nitakuwa na uhakika wana kanuni mezani*
*Zinazotoa mishahara kwa haki*
*Kwani si haki kwa anayekandamizwa kufanya kazi*
*Na mimi ninufaike*

*Nitawalinda*
*Walio katika mazingira hatarishi*
*Nitakikisha wako salama*
*Nitawalinda*
*Nitawatia moyo na sitawafumbia macho*

*Nitachunga*
*Nini nasema*
*Nitasahihisha tabia za vurugu*
*Maneno ya matusi na dharau*
*Lugha ya kudhalilisha*
*Na matumizi mabovu ya nguvu*

*Nitajitoa*
*Nijielimishe*
*Nikifahamu kwamba sio jukumu la aliyekandamizwa kunielimisha mimi*
*Kwani nisipokuwa na maarifa*
*Kuangamia hakutanishitua*